



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO  
**OFISI YA HAKIMILIKI TANZANIA**



## **TANGAZO**

### **NAFASI ZA KAZI ZA UHAMISHO KWA WATUMISHI WA UMMA**

- 1.** Ofisi ya Hakimiliki Tanzania ni taasisi ya Umma iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 7 ya mwaka 1999. Ofisi hii inafanya kazi chini ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Majukumu makuu ya Ofisi hii ni Kukuza na kulinda maslahi ya wabunifu kama watunzi, waandishi, wasanii wa fasihi, watayarishaji wa kurekodi sauti, watangazaji, wachapishaji nk., Pia Ofisi hutunza rejista ya kazi za ubunifu, kutafuta na kubainisha haki za wamiliki na kutoa uthibitisho wa hakimiliki. Aidha, Ofisi ina jukumu la kuhabarisha na kuelimisha umma kuhusu masuala ya hakimiliki na haki za wabunifu nchini, pamoja na kumshauri Waziri mwenye dhamana kuhusu masuala ya Hakimiliki nchini.
- 2.** Ofisi ya Hakimiliki inapenda kuwatangazia watumishi wote wa Umma wenye sifa na watakaopenda kujiunga na Ofisi kuwasilisha maombi yao kwa nafasi zilizo wazi ni kama ifuatavyo;
  - a. Afisa Ugavi Daraja la I-** Nafasi moja (1)
  - b. Mhasibu Daraja la II –** Nafasi moja (1)
  - c. Afisa Hakimiliki Daraja la II –** Nafasi Tatu (3)
  - d. Dereva Daraja la II –** Nafasi Moja (1)
  - e. Msaidizi wa Kumbukumbu Daraja la I-** Nafasi Moja (1)
- 3.** Vigezo vya Jumla kwa Waombaji:
  - a. Awe mwajiriwa katika Utumishi wa Umma mwenye mwenendo wa kuridhisha.
  - b. Ambatisha vyeti vya Taaluma pamoja na Transcripts na vyote viwe certified.
  - c. Ambatisha nakala ya cheti cha kuzaliwa iliyothibitishwa (Certified)
  - d. Ambatisha taarifa ya wasifu binafsi (CV).
  - e. Muombaji aweke Check Na. kwenye barua ya maombi.

f. Kwa nafasi ya Afisa Hakimiliki II, muombaji anapaswa kuwa na elimu ya Shahada ya Sheria, Masoko, Miliki Bunifu (Intellectual Property) au Usimamizi wa Biashara.

4. Watumishi wa Umma wenye sifa kwa nafasi zilizotajwa hapo juu wanakaribishwa kuwasilisha maombi yao kupitia anuani ifuatayo au kwa mtandao kupitia barua pepe iliyoainishwa hapo chini:-

Afisa Mtendaji Mkuu,  
Ofisi ya Hakimiliki Tanzania,  
Majengo ya Utumishi,  
8 Barabara ya Kivukoni,  
S.L.P 6388

**11404 DAR ES SALAAM**

Barua pepe: [barua@cosota.go.tz](mailto:barua@cosota.go.tz)

5. Maombi yote yapitishwe na waajiri wa sasa. Aidha, Ofisi haitolipa gharama za uhamisho kwa waombaji watakaopata nafasi. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 15 Mei, 2023.

6. Imetolewa na;

**Imetolewa na;**  
Afisa Mtendaji Mkuu,  
Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA),  
S.L.P 6388,  
**DAR ES SALAAM**  
**28 Aprili, 2023**